# Wananchi, redio, mbao za matangazo

## Mahitaji na upatikanaji taarifa nchini Tanzania





## 1. Utangulizi

Wananchi wanafahamu nini kuhusu watumishi na sera za Serikali, na wanatumia chanzo gani kikuu cha kupata taarifa? Je, Watanzania wengi wanahabarishwa kikamilifu kiasi cha kuweza kuwawajibisha watoa huduma? *Sauti za Wananchi*, ambao ni utafiti wa kwanza barani Afrika kwa njia ya simu za mkononi na wenye uwakilishi wa kitaifa, unajibu maswali haya na mengineyo kuhusu upatikanaji wa taarifa nchini Tanzania.

Serikali ya Tanzania hupanga na kutoa huduma za msingi ambazo huathiri maisha ya mamilioni ya wananchi. Wananchi ndio walipa kodi, na kwa sababu hiyo, wao ndio wanaobeba gharama za sera na programu za kitaifa. Wanadai na kupata huduma katika utaratibu wa kila siku, kwa mfano, katika vituo vya afya na shule. Kwa hivyo utoaji huduma za msingi huwa jambo kuu la mwingiliano kati ya Serikali na wananchi. Kuanzia ngazi ya mtaani hadi ya kitaifa, utoaji huduma za msingi unahitaji kuwapo kwa mtiririko wa taarifa na majibu ya maswali kama : Vituo vya afya vinafunguliwa kuanzia saa ngapi? Je, dawa zinapatikana? Maendeleo ya mwanangu shuleni yako vipi? Katika ngazi ya kitaifa, wananchi wanaweza kusoma kuhusu miradi ya maji inayopelekwa katika wilaya yao, wanaweza kumtumia ujumbe Mbunge wao au wanaweza kumsikiliza Waziri akitoa hotuba ya bajeti.

Ili kuelewa njia ambazo Watanzania wanapata taarifa na wanapata habari za sera za kitaifa, *Sauti za Wananchi* inawasilisha matokeo ya utafiti wa hivi karibuni kabisa wenye uwakilishi wa kitaifa kuhusu upatikanaji wa taarifa kupitia muhtasari huu. Matokeo

Matini haya yameandikwa na kutayarishwa na Uwazi ya Taweza, inayopatikana katika ofisi ya Hivos Tanzania. Imetolewa Agosti, 2013

S.L. P 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu: +255 22 266 4301 Nukushi: +255 22 266 4308.
uwazi@twaweza.org www.twaweza.org/sauti

Twaweza ni sisi

yanatokana na awamu ya tatu ya utafiti wa *Sauti za Wananchi*. Mawasiliano kwa njia ya simu yalifanyika kati ya tarehe 10 hadi 24 Mei, 2013; taarifa zinahusisha majibu kutoka kwenye kaya 1,722. Muhtasari huu pia unawasilisha matokeo ya utafiti wa msingi (mahojiano ya ana kwa ana) wa *Sauti za Wananchi* ambao uliendeshwa kati ya Oktoba na Desemba 2012 miongoni mwa kaya 2,000 kote nchini Tanzania.

Matokeo makuu yalikuwa ni pamoja na:


- Redio inaendelea kuwa chombo kikuu cha habari kinachosikilizwa na Watanzania wengi
- Ni wananchi wachache tu wenye ufahamu wa kutosha kuhusu sera za kitaifa
- Mara nyingi hakuna mbao za matangazo katika shule na maeneo mengine ya huduma
- Wananchi wangependa Serikali iweke wazi kwa umma taarifa nyingi zaidi

# 2. Mambo nane kuhusu upatikanaji wa taarifa Tanzania

## Jambo la 1: Redio inashika nafasi ya juu kati ya vyombo vya habari

Katika miezi mitatu iliyopita, asilimia 81 ya Watanzania wamesikiliza redio. Taarifa hii inaifanya redio kuwa chombo cha habari kinachotumiwa zaidi nchini. Hata hivyo, televisheni siyo tena jambo la kujidai kwa watu wenye kipato bora pekee: wananchi karibu wanafanana katika kutazama kwao televisheni (asilimia 54) kama ilivyokuwa katika kushiriki kwenye mikusanyiko ya kidini (asilimia 52) au kusoma gazeti katika miezi mitatu iliyopita. Matumizi ya intaneti bado yako chini Tanzania.

**Kielelezo cha 1: Vyombo vilivyotumiwa na Watanzania hivi karibuni kupata habari**





**Chanzo cha data:** *Sauti za Wananchi*, Utafiti kwa Simu ya Mkononi – Awamu ya 3, Mei 2013.

## Jambo la 2: Watanzania wanatumia redio ili kupata taarifa

Watanzania hutumia vyombo mbalimbali vya habari ili kupata taarifa na burudani. Kama Kielelezo cha 2 kinavyoonyesha, redio ndio iliyokuwa chanzo kilichotumiwa zaidi, kwa taarifa za jumla na kwa burudani. Mazungumzo ya ana kwa ana yanashika nafasi ya pili katika vyanzo vya kupeana taarifa. Televisheni ni chanzo cha pili kinachopendelewa katika burudani. Intaneti si chanzo muhimu cha taarifa au burudani.

**Kielelezo cha 2: Vyanzo vikuu vya Taarifa/Habari na Burudani**





**Chanzo cha data:** *Sauti za Wananchi*, Utafiti kwa Simu ya Mkononi – Awamu ya 3, Mei 2013

Hata hivyo, kama wanataka taarifa fulani, Watanzania husikiliza redio na kutafuta maoni ya wataalamu. Kwa mfano: kama wanataka ushauri wa kitabibu, asilimia 36 watasikiliza redio wakati ambapo asilimia 25 watawasiliana na watumishi wa chombo cha kutolea huduma za afya. Vivyo hivyo, kama wanataka kujua kuhusu shule bora kabisa katika wilaya yao, asilimia 33 watasikiliza redio wakati ambapo asilimia 29 watawasiliana na mwalimu mkuu au mwalimu wa kawaida. Kwa maneno mengine, watumishi wa Serikali wanaotoa huduma wana dhima muhimu katika kutoa taarifa kwa wananchi.

## Jambo la 3: Wananchi Tanzania vijijini wanajua majina ya Wabunge wao

Wabunge huchaguliwa kila baada ya miaka mitano. Wanahitajika kusimamia maslahi ya wapiga kura wao na kuwajibika kwao. Kwa kuanzia, jambo hili lina maana kwamba wananchi wanapaswa kuwafahamu wabunge wao kwa majina: je, hali kweli iko hivyo? Tanzania Bara, asilimia 81 ya wananchi wanaweza kutaja jina la mbunge wao. Kama Kielelezo cha 3 kinavyoonyesha, kiwango ni cha juu zaidi vijijini.


**Kielelezo cha 3 : Mbunge wako anaitwa nani?**




**Chanzo cha data:** *Sauti za Wananchi*, Utafiti wa Msingi, Oktoba – Desemba 2012.

**Jambo la 4: Rais Kikwete amshinda Didier Drogba (asilimia 97 dhidi ya asilimia 23)** Katika utafiti wa msingi (mahojiano ya ana kwa ana, Oktoba hadi Desemba 2012) wa *Sauti za Wananchi*, wahojiwa walitakiwa kutambua sura sita za watu maarufu kwa kutumia picha. Wananchi wengi sana (asilimia 97) miongoni mwa wahojiwa waliweza kumtambua Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa J. M. Kikwete wakati ambapo chini ya nusu yao waliweza kutambua sura zilizokuwa kwenye picha nyingine.

**Kielelezo cha 4: Je, unajua jina la mtu aliye kwenye picha hii?**





**Chanzo cha data:** *Sauti za Wananchi*, Utafiti wa Msingi, Oktoba – Desemba 2012.

## Jambo la 5: Wananchi wachache wana taarifa kamilifu kuhusu sera za taifa

Wakati ambapo Wabunge na wanasiasa mashuhuri katika ngazi ya taifa wanafahamika vema nchini Tanzania, hali ni kinyume chake kwa sera na programu za kitaifa zinazopigiwa chapuo sana zilizotungwa. Uendelevu wa utekelezaji sera na programu za kitaifa unahitaji utambuzi na uelewa wa sera hizo kwa upande wa wananchi. Hata hivyo, matokeo kutoka utafiti wa msingi (mahojiano ya ana kwa ana) wa *Sauti za Wananchi* yanaonyesha kwamba viwango vya utambuzi na uelewa wa sera ya kitaifa miongoni mwa wananchi viko chini. Kielelezo cha 5 kinaonyesha: asilimia 75 ya wahojiwa hawajawahi kusikia kuhusu mkakati wa Visheni 2025[1]. Mpango wa Kilimo Kwanza unafahamika vema zaidi ingawa wananchi hawawezi kueleza una maana gani; ni asilimia 33 tu ya Watanzania ndio wanaweza kuuelezea kwa ufasaha.

**Kielelezo cha 5: Ufahamu wa wananchi na uelewa wa sera za kitaifa**




**Chanzo cha data:** *Sauti za Wananchi*, Utafiti wa Msingi, Oktoba – Desemba 2012.


1 Visheni 2025 ni mkakati wa kitaifa unaokusudia kuhakikisha kwamba ifikapo mwaka 2025 Tanzania iwe nchi ya kipato cha kati kwa kuwa na maendeleo makubwa ya watu, na kufuta kabisa umaskini uliokithiri. Kilimo Kwanza ni azimio la kitaifa kuleta mapinduzi ya haraka ya kijani katika kilimo. MKUKUTA ni mkakati wa kitaifa wa kukuza uchumi na kupunguza umasikini.

## Jambo la 6: Mbao za matangazo hazipo, baadhi ya wananchi huuliza maswali katika vituo vya kutolea huduma

Mojawapo ya kazi kuu za mifumo ya afya na elimu ni kuwaarifu wananchi kuhusu huduma wanazopewa, kwa mfano, kuhusu dawa, muda wa kusubiri, suhula za shule na maendeleo ya wanafunzi. Je, mambo haya yanatokea nchini Tanzania?

Kielelezo cha 6 kinaonyesha kwamba asilimia 82 ya Watanzania wamehudhuria vituo vya kutolea huduma za afya. Asilimia 68 ya Watanzania walifika kwenye shule. Katika utembeleaji huu wa maeneo hayo mawili ni ule uliofanyika ndani ya wiki nne kabla ya utafiti kufanyika. Hii inaonyesha kwamba watoa huduma kwenye maeneo hayo ni watu muhimu sana kwa wananchi. Zana ya kawaida kwa ajili ya kutolea taarifa za umma ni mbao za matangazo, katika maeneo ya kutolea huduma za afya na elimu. Chini ya nusu ya wahojiwa wa utafiti wa *Sau i za Wananchi* waliofika kwenye maeneo hayo walitoa taarifa ya kuwepo kwa mbao hizi za matangazo shuleni (asilimia 35) au eneo la huduma za afya (asilimia 42) wakati walipotembelea huko. Baadhi ya wananchi huwauliza watoa huduma za afya na walimu taarifa na mara nyingi wanaridhika kwa majibu wanayopewa.


**Kielelezo cha 6: Taarifa katika maeneo ya kutoa huduma za afya na elimu yaliyotembelewa**




**Chanzo cha data:** *Sauti za Wananchi*, Utafiti kwa Simu ya Mkononi – Awamu ya 3, Mei 2013.

Wananchi wanataka kujua nini zaidi? Je, mbao za matangazo zinahitajika? Kama ilivyoonyeshwa katika Kielelezo cha 7, wale waliotembelea shule ya msingi au sekondari wana shauku ya kupata taarifa kuhusu mambo kama vile ukusanyaji wa mapato, fedha za ruzuku kwa wanafunzi na matumizi ya shule (asilimia 28), menejimenti na upatikanaji wa zana shuleni (asilimia 18).

**Kielelezo cha 7 : Aina ya taarifa wananchi wanazotaka kupata shuleni**





**Chanzo cha data:** *Sauti za Wananchi*, Utafiti kwa Simu ya Mkononi – Awamu ya 3, Mei 2013.

## Jambo la 7: Wananchi maskini wanaona kwamba huduma za afya ni duni sana

Utafiti wa *Sauti za Wananchi* uliwataka wahojiwa kulinganisha ubora wa huduma za afya wanazopata na zile wanazopata Watanzania wengine. Katika muhtasari huu, tunatazama majibu yaliyotolewa na wahojiwa kutoka kundi la matajiri sana na wale walio maskini sana wanaoshiriki utafiti wa *Sauti za Wananchi*. Matokeo yaliyo katika Kielelezo cha 8 yanaonyesha kwamba kwa kundi la matajiri[2] hakuna mwenendo unaofahamika vizuri: wana nafasi ile ile ya ama kujisikia kupata huduma bora au hafifu kulinganisha na Watanzania wengine. Miongoni kwa maskini, karibu nusu yao (asilimia 47) wanasikia kuwa wanapata huduma dhaifu kuliko Watanzania wengine. Hata hivyo, kuna wahojiwa maskini wanaojisikia kuwa na unafuu kulinganisha na Watanzania wengine pale linapokuja suala la huduma za afya.

2 Wahojiwa wa makundi ya tajiri zaidi na maskini zaidi wanabainishwa kwa kutumia faharisi ya utajiri ambayo inakokotolewa kwa kutumia umiliki katika kaya wa mali zilizoteuliwa, ambalo kwalo asilimia 20 ya wahojiwa wenye umiliki wa juu zaidi wa mali hizo zilizoteuliwa wako kundi la matajiri zaidi wakati asilimia 20 ya wahojiwa wenye kiwango cha chini zaidi cha umiliki wa mali hizo wako kundi la maskini zaidi.

**Kielelezo cha 8: Kwa kulinganisha ubora wa huduma za afya walizopata wengine nchini Tanzania, je, mawazo yako kuhusu ubora wa huduma ya tiba uliyopata ni nini?**





**Chanzo cha data:** *Sauti za Wananchi*, Utafiti kwa Simu ya Mkononi – Awamu ya 3, Mei 2013.

## Jambo la 8: Wananchi wanataka taarifa zaidi ziwekwe hadharani

Utafiti wa *Sauti za Wananchi* uliwauliza wahojiwa kama kuna taarifa ambazo wangependa Serikali iziweke hadharani. Wananchi (asilimia 42) wana shauku ya kupata taarifa zaidi kuhusu masuala mbalimbali kama inavyoonyeshwa kwenye Kielelezo cha 9. Mada zenye mvuto zaidi ni zile zinazohusu elimu; uchumi na maendeleo; katiba; huduma za afya na maji; uongozi wa nchi na rushwa.

**Kielelezo cha 9: Taarifa ambazo wananchi wangependa Serikali iziweke wazi hadharani**




**Chanzo cha data:** *Sauti za Wananchi*, Utafiti kwa Simu ya Mkononi – Awamu ya 3, Mei 2013.

## 3. Hitimisho

Muhtasari huu unaonyesha kwamba Watanzania wengi wanaonyesha kuwa na kiu cha kupata taarifa na data zaidi kutoka Serikali. Wananchi hasa wanataka taarifa kuhusu upatikanaji wa huduma kama vile elimu, maji na afya lakini pia kuhusu utawala na uchumi. Zaidi ya hilo, muhtasari huu unaonyesha kwamba siasa kwa Watanzania walio wengi ni kuhusu watu wachache (Mbunge wao, Rais), hasa vijijini: idadi kubwa kabisa ya wananchi walio wengi (asilimia 97) wanaweza kutambua sura ya Rais wa Tanzania lakini ni wachache tu walio na utambuzi na wanaoweza kueleza masuala makuu ya sera. Yaelekea kwamba wanasiasa wanafunika masuala ya sera, kama ilivyo katika nchi nyingi.

Katika maeneo wanakoishi watu, chini ya asilimia 50 ya wahojiwa waliotembelea ama kituo cha afya au shule ya msingi/sekondari waliripoti kuona mbao za matangazo katika maeneo hayo. Kukosekana huku kwa mbao za matangazo kunaonyesha suala zito zaidi: utoaji taarifa za umma hakupewi kipaumbele na hautokei kwa utaratibu uliowekwa, ingawa ni jambo la lazima. Jambo hili linawaacha wananchi gizani kuhusu viwango vya huduma kwa kuwa hawajui viwango gani vya huduma wategemee na gani wasitegemee. Matokeo yanayohusiana na hali hiyo ni kwamba watu wengi wanajihisi kupata huduma mbaya zaidi kuliko wengine. Uwazi katika ngazi ya kitaifa kuhusu ubora wa utoaji huduma utaziimarisha na unaweza kupunguza mivutano kwa kuhimili matarajio kuhusu viwango vya huduma vinavyotarajiwa.

Mwisho, muhtasari unaainisha maeneo na mada ambazo wananchi wanaitaka Serikali ya Tanzania kuzitolea taarifa na data zaidi, zikiwamo huduma za msingi (elimu, afya na maji), uchumi na utawala. Kwa bahati nzuri, Tanzania ni moja ya nchi zilizotia saini Mpango wa Kimataifa wa Kuendesha Shughuli za Serikali kwa Uwazii (OGP), ambao ni jitihada ya ulimwengu unayolenga kuhamasisha uwazi, kuwapa wananchi nguvu zaidi, kupiga vita rushwa na kuhamasisha matumizi ya teknolojia mpya kuongeza ufanisi katika utawala. Jambo hili lina maana kwamba, nchini Tanzania kuna mahitaji zaidi ya taarifa za umma na pia utayari wa Serikali kuhakikisha upatikanaji wake. Utafiti wa *Sauti za Wananchi* utafuatilia, kupitia tafiti za kila baada ya muda fulani, maendeleo ya upatikanaji wa data kwa wananchi.